# Istiara katika Riwaya ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert

*Alfred Malugu*
*Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agostino cha Tanzania*

**Ikisiri**

**Makala haya yanakusudia kuonesha jinsi istiara ilivyotumika katika riwaya ya mwandishi nguli Shaaban Robert ambaye ni mmojawapo wa waandishi maarufu na waliosifika sana katika utunzi wa kazi mbalimbali za fasihi. Shaaban Robert aliiandika riwaya yake ya Kusadikika mnamo mwaka 1951. Utunzi wa kazi za fasihi kwa kutumia mbinu ya istiara ulikuwa/umekuwa nyenzo muhimu sana katika kuusawiri, kuubeza na kuukosoa mfumo wa kikoloni na pia hata mfumo mwingine wowote ule ambao unaonekana kwenda kinyume na matakwa ya jamii fulani. Kwa kuwa Shaaban Robert ni miongoni mwa watunzi wa kazi za fasihi walioanza kuandika kazi zao katika kipindi cha ukoloni, tumeona ni vyema tukaangalia ni kwa vipi mtunzi huyu ametumia mbinu hii ya istiara kama mbinu mojawapo za kiutunzi zenye lengo la kusawiri hali halisi katika jamii hususan katika kipindi cha ukoloni. Kwa hivyo basi, makala yatajikita katika kuangalia dhana ya istiara na jinsi ndugu Shaaban Robert alivyotumia istiara katika riwaya hii na pia kufafanua maana zinazoweza kupatikana kutokana na matumizi hayo ya istiara. Katika kufanikisha uchambuzi huu, makala haya yatatumia nadharia ya udenguzi kama ilivyoasisiwa na Derrida (1967).**

**Maneno Muhimu:** Istiara, Riwaya, Kusadikika, Shaaban Robert

## Utangulizi

Riwaya ya *Kusadikika*, ni miongoni mwa riwaya za mwanzo kabisa za mwandishi Shaaban Robert. Kulingana na Chuachua (2011), riwaya hii inasemekana ilitungwa mwaka 1948 na kuchapishwa 1951. Riwaya hii ni pacha wa *Kufikirika* kimaudhui. Kifani ni nyepesi kuliko *Kufikirika*. Kusadikika ni jina lililotumika kurejelea tafsiri ya neno 'sadiki' lenye maana ya 'amini.' Kwa hiyo, Kusadikika maana yake ni ya 'kuaminika'. Chuachua (*keshatajwa*) anafafanua kuwa, maudhui yanayochimuza katika kazi hii yanadhihirisha kuwa, jina hili halikutumika kwa mtazamo chanya, bali ni kiudakuzi. Utawala wenye taasubi za kikoloni, wa Kusadikika, unadakuliwa na mwandishi kwa kuonyesha ghaidhi aliyo nayo dhidi yake.

Aidha, Herman (2012) anazungumzia kuwapo kwa matumizi ya fantasia katika fasihi ya watu wazima ambapo matumizi haya huleta upya fulani ambao unakuwa haujazoeleka na hivyo kuwashtua wahakiki wa fasihi. Akimnukuu Senkoro (2006), Herman anadai kuwa mshtuko huo ndio uliozaa istilahi ya "uhalisiamazingaombwe" yaani zile kazi zinazounganisha uhalisi na uajabuajabu.

Akiendelea kumnukuu Senkoro, Herman (*keshatajwa*) anasema kuwa upya huu unaonekana pia katika kazi za Shaaban Robert kama vile *Kusadikika*, *Kufikirika* na *Adili na Nduguze*.

Matumizi ya mbinu hii ya uhalisiamazingaombwe katika riwaya ya *Kusadikika* yalikuwa na nafasi muhimu katika kujenga istiara na hivyo kufikisha ujumbe kama mwandishi alivyokuwa amekusudia. Mulokozi (2017) katika kuelezea riwaya za kiistiara, anadai kuwa, yaelekea riwaya ya Shaaban Robert, *Kusadikika* (Nelson 1951) ni istiara kuhusu utawala wa mabavu wa kikoloni. Vilevile, Senkoro (2011), anafafanua kuwa, (istiara) tamathali hii huwa ni masimulizi yatumiayo ishara ambayo maana yake hujitokeza pia katika masimulizi mengine. Istiara basi, ni aina moja ya tamathali ya kisitiari ambayo imepanuka zaidi katika matumizi."

Mulokozi (2017) katika kuelezea maana ya riwaya ya istiara anadai kuwa, "Ni riwaya ya mafumbo ambayo umbo lake la nje ni ishara au kiwakilishi tu cha jambo jingine. Kwa upande wake Mlaga (2013) anazitaja riwaya za *Kufikirika* na *Kusadikika* kuwa miongoni mwa riwaya fiche ambazo zinaweza kutazamwa kama riwaya zinazoelezea historia halisi ya kipindi cha ukoloni kwa namna ya uficho.

Malezo hayo ya wataalamu tuliowapambanua hapo juu yanadhihirisha dhahiri kabisa kuwa, riwaya ya *Kusadikika* iliandikwa kwa mtindo au mbinu fulani ya uficho. Mbinu hii ambayo ni ya kiistiara ilitumika kama mbinu mahsusi ya kuusawiri, kuukosoa au kukejeli mfumo fulani wa kiutawala ambao pengine ulionekana hautendi haki kwa wananchi. Utawala wa kikoloni ulikuwa mojawapo ya tawala ambazo hazikutenda haki kwa wananchi hususani wale waliowatawala. Kwa hivyo, Shaaban Robert kupitia riwaya yake ya *Kusadikika* alijaribu kuushambulia mfumo wa utawala wa kikoloni kwa kutumia mbinu ya istiara.

**Historia Fupi ya Shaaban Robert**

Tukimrejelea Chuachua (2011) anadai kuwa, jina la mwandishi huyu limezua mitazamo tofauti tofauti kwa kuwa limejumuisha majina mawili yenye asili ya Uislamu (Shaaban) na lingine ya Ukristo (Robert). Wapo waliodhani kuwa amejiita hivyo ili kuonyesha msimamo wake wa kati kuhusu dini, kuwa dini zote zina hadhi sawa. Wengine wameeleza kuwa jina la Robert ni la Mtaliano aliyekuwa mwajiri wa baba yake mzee Selemani Ufukwe.

Inasemekana kuwa, jina halisi la baba yake Shaaban Robert ni Lubeti ambalo bila shaka ndilo lililopata athari ya kimatamshi na kuwa Robert. Watu wengi wameandika kuhusu maisha yake lakini kwa bahati mbaya taarifa kuhusu tarehe ya kifo chake imekuwa ikikosewa mara kwa mara. Tarehe ya kuzaliwa kwake haiyumbishwi. Karibu wote wameandika tarehe 1. 1. 1909 bila shaka, hii ni tarehe sahihi. Chuachua (*keshatajwa*) akiwarejelea baadhi ya watafiti (Gibbe 1978; Kezilahabi 1976) anasema kuwa, watafiti hawa wanadai kuwa Shaaban Robert alifariki tarehe 22. 6. 1962 akazikwa Machui. Kulingana na utafiti alioufanya (Chuachua) kupitia kwa mtoto wa marehemu Shaaban Robert ajulikanaye kama

Ikbal, Shaaban Robert unaonyesha kuwa, Shaaban Robert alifariki tarehe 20. 6. 1962 na kuzikwa huko Vibambani tarehe 21. 6. 1962. Mtafiti huyu anatushawishi tukubaliane na taarifa alizozipata kutoka kwa mtoto wa marehemu kwa kuwa mwanawe huyo alishuhudia kufa na kuzikwa kwa baba yake. Inasemekana kuwa, kabla ya kifo chake, makazi yake ya awali yalikuwa Barabara ya Tisa, Tanga Mjini.

Aidha, inasemekana kuwa, mwandishi huyu alianza kuandika huku akiwa hakwenda mbali kielimu. Alianza shule mwaka 1922 na kumaliza 1926 mjini Dar es Salaam katika shule ya Kichwele (Uhuru Mchanganyiko). Licha ya elimu yake ndogo bado aliweza kujipambanua mapema kama mwandishi mashuhuri. Hata hivyo, jitihada zake za kufika mbali kielimu hazikuzaa matunda kwa haraka, ziliporwa na wakoloni kwa lengo la kumtumia kama chombo cha kutawalia. Hata hivyo, mwaka 1932 aliendelea na masomo kwa njia ya posta ambapo mwaka 1934 alitunukiwa Diploma ya Fasihi. Mwaka 1936 – 37 alitunukiwa cheti cha English Level. Pamoja na harakati za kielimu alizozionesha, alipata kupitia masomo ya dini (madrasa) ambapo alipelekwa na mama yake mzazi alipokuwa na umri usiozidi miaka tisa.

Ilipofika mwaka 1926, alianza kazi katika Idara ya Forodha Tanga. Hapo alidumu kwa muda wa miaka takribani 18. Kati ya mwaka wa 1944 -1946 alihamishiwa Idara ya Wanyamapori huko Mpwapwa. Mwaka 1946 alirudishwa Tanga na kuwa Afisa Ardhi wa jimbo la Tanga. Aidha, barua zake zinaonyesha kuwa alifanya kazi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Pwani (Dar es Salaam na Kisiju). Kufanya kwake kazi chini ya utawala wa kikoloni ni ithibati kubwa ya umahiri na uaminifu wake katika utendaji kazi.

Maisha yake ya kazi yalivuka mipaka ya utumishi wa serikali ya kikoloni kwa manufaa yao hadi kwenye shughuli za kukuza na kukiendeleza Kiswahili kwa manufaa ya wazawa. Hakuchelea kuwa mwanachama wa East African Swahili Committee, East African Literature Bureau na Tanganyika Language Board. Shaaban Robert alikuwa mwenyekiti wa Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki kutoka Novemba 1961 hadi alipofariki 1962. Kutokana na uandishi wake, Waingereza walimtunuku nishani ya M.B.E yaani "Member of British Empire" (Mwanachama wa Dola ya Uingereza) na zawadi ya uandishi inayoitwa "Margret Wrong Memorial Prize."

**Nadharia na Istiara**

Wataalamu wa tasnia mbalimbali kama vile isimu, fasihi, sanaa, falsafa, theolojia na nyinginezo kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakiifungamanisha istiara sanjari na muktadha mahsusi. Kimsingi, katika makala haya, istiara itafafanuliwa na kutazamwa tofauti na ambavyo ingeweza kutazamwa kama taswira au tamathali nyingine za semi kama vile tashbiha, tashihisi, mbazi au ishara. Wakati ambapo katika tamathali za semi na taswira maana huweza kupatikana katika neno, katika istiara maana hupatikana kwa kiwango cha miundo au usimulizi. Istiara huweza kufahamika vizuri zaidi hususani pale tunapoichambua kazi ya fasihi kwa kurejelea

nadharia ya udenguzi; nadharia ambayo msingi wake unatokana na mawazo ya Jacques Derrida (1967). Kulingana na mawazo ya wafuasi wa nadharia hii, huwa hakuna maana moja ya matini. Kwa maana nyingine vipengele mbalimbali vinavyounda matini husababisha kuwepo walau na maana zisizopungua mbili katika matini.

Katika nadharia ya udenguzi kama ilivyoasisiwa na Jacques Derrida (1967), Udenguzi unapingana moja kwa moja na umuundo na mitazamo mingine inayoichukulia lugha na fasihi kuwa miundo inayojitawala. Wafuasi wa nadharia hii huamini kuwa muundo wa lugha na fasihi huendelea kubadilika. Kwa upande wa fasihi, hii ina maana kwamba kila usomaji wa kazi ya sanaa ni toleo jipya la kazi hiyo. Kutokana na madai ya udenguzi, hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Hii ndiyo sababu inayowafanya wahakiki kutoa fasili tofautitofauti kwa jambo lilelile moja ambapo baadhi ya fasili hizo zinapingana zenyewe kwa zenyewe, maadamu tu kunakuwepo na ushahidi wa kutosha. Derrida (keshatajwa) aliamini kuwa neno lililopo huendelea kuahirisha maana yake ya mwisho. Jambo hili huifanya maana kukosa utangamano. Waitifaki wa udenguzi kama vile J. Hills Miller (1967) wanasema kwamba udenguzi hauivunji kazi ya fasihi katika vipande vipande na kinyume chake ni kwamba, nadharia hii ni nadharia inayosawiri kwamba kitambo kazi ya fasihi imejivunja yenyewe (Wafula na Njogu, 2007). Kimsingi, nadharia hii ya udenguzi ni mahsusi kabisa hasa katika kuichambulia riwaya hii ya *Kusadikika* huku tukijiegemeza katika kutazama jinsi matumizi ya istiara yalivyofanikisha kuwasilisha maudhui ya kitabu hiki kwa kipindi hicho cha miaka ya 1950 ambacho kilikuwa ni kipindi cha ukoloni.

**Istiara Zinazopatikana katika Riwaya ya *Kusadikika***

Katika sehemu ya utangulizi wa riwaya hii, Kusadikika inasawiriwa kama ifuatavyo:

> *Kusadikika ni nchi ambayo kuwako kwake hufikirika kwa mawazo tu. Nchi hiyo iko katikati ya mipaka sita. Kwa upande wa Kaskazini imepakana na Upepo wa Kaskazi, na kwa upande wa Kusini imepakana na Upepo wa Kusi. Mashariki imepakana na Matlai, na Magharibi mpaka wake ni Upepo wa Umande. Kwa kuwa nchi yenyewe inaelea katika hewa kama wingu, zaidi ya kupakana na pepo nne hizo, ina mipaka mingine miwili. Mipaka yenyewe ni hii. Kwa juu nchi hiyo imepakana na Mbingu, na kwa chini imepakana na Ardhi* (*Kusadikika*:Utangulizi).

Maelezo hayo hapo juu, yanatutanguliza katika kile tunachoenda kukijadili hususani nchi ya Kusadikika sanjari na bara la Afrika. Tukumbuke kwamba, hapo awali kabla ya watangulizi wa kwanza kutoka Ulaya na kuzuru Afrika, haikuwepo dhana ya kwamba kuna bara kama hili. Habari kuhusu Afrika zilikuwa ni za kufikirika tu. Kuwapo kwa mipaka sita tofauti na ilivyozoeleka kwamba nchi zote

duniani hupakana katika pande sita tu ni uthibitisho wa kustaajabisha kabisa uliohusishwa na bara la Afrika.

Aidha, akifafanua zaidi, Shaaban Robert anaendelea kutupa picha halisi ya nchi hiyo ya Kusadikika kwa kutuonesha sifa ya wanawake waliokuwa wakipatikana katika nchi ya Kusadikika kwa kusema:

> *Wanawake wote katika nchi hiyo huzaa watoto pacha. Hii ni habari ya ajabu sana lakini haionekani kuwa imepata kugusa ndoto za wazee. Wasimulizi bado kuisimulia, wala haijawashawishi wapima kuitia nchi hiyo katika ramani. Labda kukosekana kwa habari za nchi hiyo katika ndoto za wazee, katika masimulizi na katika ramani kutafanya udhuru wangu wa kuisimulia hadithi yake kukubalika* (*Kusadikika*: Utangulizi)

Tukiangalia kwa jinsi ambavyo mwandishi huyu kwanza alivyojaribu kuisawiri nchi ya Kusadikika na mahali ilipokuwa, yaani Kusadikika kama nchi iliyokuwa ikielea kama hewa na huku ikiwa na mipaka sita, pengine maelezo haya tunaweza kuyatazama kama istiara iliyotumika kulisawiri bara la Afrika, bara ambalo hapo awali kabla ya kuja kwa wageni liliitwa bara la giza. Kutopatikana kwa taarifa za kutosha kuhusu bara hili ambako ndiko kulikolifanya litazamwe kama bara la giza kunaenda sambamba na maelezo kuwa habari hizi kamwe hazijapata kuzigusa ndoto za wazee. Pengine wazee tunaweza kuwafananisha na wakoloni au watu wa Ulaya ambao kwa kukosa kwao taarifa za kutosha hata pale waliposikia mambo mazuri ikiwemo utajiri wa kila aina katika ardhi ya nchi za Afrika, hawakuwa tayari kuamini bali waliamini kuwa mambo na vitu vyote vizuri kamwe haviwezi kupatikana katika bara la Afrika. Kuwapo kwa nchi ambayo wanawake wake wote huzaa pacha kunaweza kufananishwa na kuwapo bara au nchi isiyojulikana ambayo ina utajiri wa rasilimali za kila aina. Mawazo kama haya ya kuwapo kwa rasilimali za kutosha katika bara la Afrika pengine hayakuwahi kufikiriwa kabisa na watu wa mataifa ya Ulaya. Leo hii tunapolitazama Bara la Afrika na kwa jumla tunaona jinsi kunavyopatikana rasilimali mbalimbali kama vile, madini, mafuta, gesi wanyama na viumbe wengine wa kupendeza, vitu ambavyo hapo awali havikuweza kufikiriwa kama vingeweza kupatikana Afrika.

Tukirejelea vitabu mbalimbali vya historia tunakutana na mawazo ya wanahistoria mbalimbali waliotoa mawazo kama haya. Miongoni mwa wataalamu hao ni George Hegel ambaye alidiriki kuliita Bara la Afrika kuwa ni bara la giza. Hegel kwa kutokuwa na taarifa za kutosha kuhusu bara la Afrika alidiriki kuliita bara la Afrika kuwa ni bara la giza akiamini kuwa hakuna jambo lolote zuri linaloweza kupatikana katika bara la Afrika. Kwa hivyo, analitazama bara la Afrika kama bara ambalo wananchi wake wamo gizani katika masuala ya kiuchumi, kiutawala, kiutamaduni na kadhalika kiasi kwamba iliaminika kuwa Afrika ni bara lisilokuwa na utamaduni wala ustaarabu wowote ule.

Hapana shaka kuwa, usawiri huu wa nchi ya Kusadikika na mipaka yake na kutazamwa kwake kama ni nchi ambayo kuwepo kwake ni kwa kufikirika tu, ni

sawa na mawazo yaliyokuwa yamejengeka na bado baadhi ya watu kutoka nchi za Ulaya na Amerika wanayo vichwani mwao.

Mbali na istiara hizo zinazopatikana mwanzoni mwa sehemu ya utangulizi wa kitabu, istiara nyingine tunayoweza kuipata katika kitabu hiki inafungamana na maelezo yafuatayo:

> *Waziri wa Kusadikika alikuwa ni mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mwingi. Kwa hivi aliitwa Majivuno… Umri wake mkubwa ulizifanya nywele zake kichwani kuwa nyeupe kama fedha…* (uk.1)

Mwandishi anajaribu kumsawiri Majivuno; waziri mkuu wa nchi ya Kusadikika kama mtu aliyekuwa na majivuno sana sawa na jina lake lilivyo. Kukaa kwake madarakani kwa muda mrefu pamoja na mvi zake kichwani, kulimfanya aweze kuamini kuwa watu wenye mvi tu ndio watu wanaoweza kuwa na hekima na wale wenye nywele nyeusi katu hawawezi kuwa na hekima na hata weusi wa nywele zao ni ishara ya ujinga walio nao akilini mwao. Dhana hii ya kuulinganisha weusi wa Waafrika kuanzia nywele zao hadi rangi zao za mwili kwa kuufungamanisha na kutokuwa na hekima au uwezo wa kuibua mawazo mazuri na yenye tija yaliibuliwa na watu weupe (wazungu). Hawa walichukulia weupe wa nywele zao kama uwezo mkubwa wa kufikiri zaidi ya watu wenye nywele nyeusi (Waafrika) ambao weusi wa nywele zao ulitazamwa kama ujinga waliokuwa nao. Hapa mwandishi anatuambia kuwa:

> *Waziri alitaka shauri la mshitakiwa likatwe siku ile ile… Hekima ni kitu adimu kupatikana kwa mtu asiye na mvi. Weusi wa nywele za mshitakiwa waonyesha waziwazi ujinga alionao. Nataka athibitishe kama nisemayo si kweli* (uk.10).

Kwa madai hayo hapo juu, waziri mkuu ndugu Majivuno hakutaka mfalme wa nchi ya Kusadikika akubali kumpa nafasi ya kujitetea Karama baada ya kuwa ameshtakiwa kwa kuanzisha taaluma ya uanasheria. Hoja ya msingi ya Waziri Majivuno iliegemea kulekule, kwamba haiwezekani mtu mwenye nywele nyeusi (Mwafrika) akawa na mawazo yenye tija bali mawazo yenye tija yalipaswa yatolewe na mtu mwenye mvi (mvi zikimaanisha nywele nyeupe yaani mzungu). Lengo la Karama kuanzisha taaluma hiyo ya uanasheria lilikuwa kuwaelimisha Wasadikika kuhusu haki zao. Licha ya kuanzishwa kwa taaluma hii ya sheria ambayo ilikuwa na lengo jema kwa Wasadikika, waziri Majivuno anaifasili taaluma hii kuwa ni taaluma iliyoanzishwa ili kupingana na sheria za Kusadikika na hivyo waziri huyu akafungua mashtaka dhidi ya mhusika Karama. Kutokana na mtuhumiwa kuwa na nywele nyeusi, Majivuno hakuamini kuwa mtu mwenye nywele nyeusi anaweza kuibua wazo jema au kufanya shauri jema. Maelezo haya yanashadidiwa na nukuu ifuatayo:

> *Jalali Mfalme na madiwani wakuu, mtakumbuka kuwa tangu zamani matendo makubwa yoyote yaliamriwa kuanzishwa na kutendwa na watu wenye nasaba bora kama wafalme na madiwani. Watu ovyo kama alivyo*

*mshtakiwa hawakuachiwa kujishughulisha na mambo yaliyo zaidi ya yale yaliyohusiana na maisha yao wenyewe tu. Kama wangaliamriwa kujishughulisha na mambo yaliyowapita vimo vyao, kama mshtakiwa aonekanavyo kuwa ndilo kusudi lake, mabadiliko ya kuchukiza yangalikuwako mara kwa mara katika nchi* (uk.4).

Kulingana na dondoo la hapo juu, mwandishi anatuonyesha ile dhana iliyokuwa imejengwa na wazungu kuhusu kufanya maamuzi mazito. Katika kipindi cha ukoloni, Waafrika hawakupewa nafasi ya kujadili au kuanzisha mambo makubwa yaliyoaminika kutumiwa kama mwongozo katika jamii zao. Kwa mfano hata katika masuala ya kiutawala, nafasi zote za juu zilizohitaji maamuzi makubwa zilikuwa ni kwa ajili ya wazungu. Waafrika waliachiwa nafasi za chini ambazo kimsingi watu weupe walizipuuza na kuziona hazikuwa za hadhi yao. Katika dini za kikristo, ibada maalumu kama vile za ubatizo na kipaimara ziliongozwa na mapadri wa kizungu ilhali mafundisho ya watoto wadogo kama vile kufundisha Katekisimu kwa ajili ya kuwaandaa watoto hao kwa ajili ya ubatizo na kipaimara kwa Wakatoliki shughuli hiyo waliachiwa Makatekista wa Kiafrika. Kiistiara, mashtaka juu ya Karama na hata kitendo cha kuzuiliwa kujitetea mahakamani kinaweza kunasibishwa na mawazo tuliyokwisha kuyatoa hapo awali kuwa, katika kipindi cha ukoloni Mwafrika (Mtu mwenye nywele nyeusi) hangeweza kutazamwa kama mtu mwenye uwezo wa kuanzisha jambo lenye manufaa kwa watu wote wakiwamo wakoloni na kwa hivyo iliaminika kuwa ni mkoloni (mtu mwenye nywele nyeupe) tu ndiye mwenye uwezo wa kuanzisha mawazo yenye tija. Kwa hivyo, Waafrika walipaswa kusubiri na kupokea mawazo kutoka kwa wakoloni. Hapana shaka kuwa, kwa mtazamo huu ndio maana walipokuja wakoloni walianzisha mambo mengi mapya kwa Mwafrika ambapo Mwafrika alitakiwa kuyaiga kutoka kwa wakoloni. Kwa mfano, Mwafrika alipaswa kupuuza imani yake ya asili na kufuata imani ngeni kama ile inayotokana na dini ya kikristu, kwa upande wa taaluma, Mwafrika alipaswa kuachana na mfumo wake wa elimu iliyokuwa ikitolewa kwa njia ya mdomo na vitendo na huku ikichukuana na mahitaji na mazingira ya walengwa na badala yake Mwafrika akalazimika kufuata elimu ya kigeni ambayo pengine haikuwa ikichukuana na mahitaji pamoja na mazingira yaliyomzunguka. Hivyo basi, wakoloni kwa upande wa elimu, walileta vitabu kutoka Ulaya na kuvifasiri ili vitumike kufundishia, vitabu ambavyo kimaudhui havikuwa vikichukuana na utamaduni wa Mwafrika bali utamaduni wa mzungu. Mfano wa vitabu hivi ni kama vile *Mashimo ya Mfalme Suleimani, Kisiwa chenye Hazina*, *Hadithi za Allan Quartermain* na vingine vingi. Yote haya yalifanyika ili kutimiza kile kilichoaminiwa na waziri mkuu Majivuno kuwa mtu mwenye nywele nyeusi hawezi kuibua jambo lolote lenye manufaa bali mtu mwenye mvi/nywele nyeupe.

Vilevile, kuna istiara inayojitokeza kupitia kwa wajumbe mbalimbali waliojitolea kusafiri kutoka nchi ya Kusadikika na kwenda kujifunza maendeleo yaliyokuwa yamefikiwa na nchi nyingine zilizokuwa zikipakana na nchi hii. Wajumbe hawa ni kama vile Buruhani, huyu alikuwa mjumbe aliyejitolea kwenda

Kaskazini, Fadhili ni mjumbe aliyejitolea kwenda Mashariki/Matlai, Kabuli alijitolea kwenda Kusini, Auni alijitolea kwenda Magharibi, Ridhaa alijitolea kwenda Mbinguni, ambapo Amini yeye alijitolea kwenda Ardhini. Kujitolea kwa wajumbe hawa kunafananishwa na safari za kujitolea zilizofanywa na watu mbalimbali kutoka katika bara la Ulaya kwa manufaa ya mataifa yaliyowatuma. Kulikuwapo na makundi ya watu mbalimbali waliojitolea kusafiri kwenda sehemu mbalimbali duniani. Makundi haya ni kama yale ya wamisionari, wapelelezi na wafanyabiashara. Kwa kuwataja kwa majina baadhi yao ni kama vile wakina Bathromeo Diaz, Vasco Da Gama, Christopher Columbus, Dr. Livingstone, Henry Morton Stanley, John Speke na wengineo.

Katika safari hizi za kujitolea kwa wajumbe hawa wa kutoka bara la Ulaya, tunaambiwa kwamba walikumbana na masaibu mbalimbali kama vile kufa kwa magonjwa kama vile mafua na malaria, baadhi yao walishambuliwa na wanyama wakali au makabila makali wakati wakijaribu kujipenyeza ili waweze kufika katika maeneo mbalimbali kwa minajili ya kujifunza mambo kadhaa na hatimaye warejeshe taarifa hizo barani kwao. Historia inatuambia kuwa ujio wa wageni kutoka Ulaya ulikumbana na changamoto kama vile kuliwa na samba wa Tsavo au kushambuliwa na makabila kama vile Wamasai na makabila mengine mengi ya Kiafrika. Mwandishi Shaaban Robert anazinasibisha safari hizi sawa na zile zilizofanywa na wajumbe kwa kujitolea kutoka katika nchi ya Kusadikika na kwenda katika nchi nyingine kujifunza maendeleo yaliyokuwa yamefikiwa na mataifa hayo. Kwa mfano anamtumia mjumbe wa Kaskazini aliyejulikana kama Buruhani kutuonesha masahibu aliyokumbana nayo mjumbe huyu, anasema:

> *Buruhani alikuwa mtu mwenye sifa zilizotakiwa na zaidi. Alitokea wakati nchi yake ilipomtaka sana akajitwisha mzigo mzito sana. Kazi yake ilikuwa kusafiri, kutalii na kuandika habari za mambo ya nchi ngeni aliyoyafikiri kwamba yaliweza kuistawisha Kusadikika. Ujumbe huu ulikuwa na dhima kubwa. Kama zamani wasafiri walivyojusurisha kuondoka katika nchi walizozijua na kusafiri katika nchi walizokuwa hawazijui, msafiri huyu pia alikujua alikotoka lakini hakukujua alikokwenda. Hakujua kama mbele alikuwa akingojewa na msaada wa kumsaidia au maangamizi ya kumwangamiza* (uk. 13).

Kwa kupitia maelezo hayo ya mwandishi, hapana shaka kuwa kile tunachoelezwa katika vitabu vya historia kuwa miongoni mwa mambo waliyokumbana nayo wamisionari, wapelelezi na wafanyabiashara kutoka Ulaya wakati wakija Afrika ilikuwa ni pamoja na kujikuta wengine wakipotea na hatimaye kutokea kule ambako hawakuwa wamekutarajia, mfano halisi ni Vasco Da Gama aliyepotea njia wakati akitafuta njia ya kwenda India na hatimaye kujikuta ametokezea Rasi ya Tumaini Jema (Cape of Good Hope). Hii inatudhihirishia kuwa watu hawa walifahamu walikotoka lakini hawakuwa wanafahamu walikokuwa wakienda.

Istiara nyingine inayojitokeza ni ile inayosawiriwa kupitia kwa Kabuli. Mjumbe huyu alijitolea kwenda Kusini. Katika safari yake, mjumbe huyu anaangukia mikononi mwa Majuju ambalo ni taifa lafi na litishalo kabisa. Hapo awali mjumbe huyu baada ya kukamatwa na Majuju, Mfalme Jeta alitaka kumla Kabuli bila kugawana na wenzake na hatimaye pakatokea vita vikali miongoni mwao hali iliyosababisha kila kitu kilichokuwa hai kuangamizwa na akabakia Kabuli peke yake. Baada ya tukio hilo, Kabuli alinusurika katika tukio jingine katika nchi ya Hasira, nchi ya watu wakali kabisa. Katika kuthibitisha haya, mwandishi anatuambia:

> *… Mara mbili alikamatwa akafanywa mahabusi. Mara ya kwanza alikamatwa Juju, nchi ya Mfalme Jeta. … Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amekaa kitako mdomo wazi. … Mfalme alitaka kumla Kabuli bila ya kugawana na wawinda waliomkamata…*
>
> *Baada ya kushukuru uwezo uliomwokoa, Kabuli aliendelea katika safari yake mpaka akafika Hasira, nchi ya watu wakali kabisa. Huko alikamatwa tena akashtakiwa kwamba alikuwa mjasusi aliyeingia katika nchi bila ya idhini. … Basi alihukumiwa kwanza, kulichimba kaburi lake mwenyewe; pili, likiisha ajilaze mwenyewe juu ya ukingo wake ili afungwe kwa pingu mikononi na miguuni; na tatu, shingo yake ikerezwe kwa msumeno kidogo kidogo mpaka mshipa wa mwisho ukatike ndipo atumbukizwe kaburini na kufukiwa. Ulinzi wa askari wawili wenye silaha ulikuwa juu yake.* (kur. 25-26)

Madondoo hayo mawili yanashadidia jinsi istiara ilivyotumika katika riwaya ya *Kusadikika* na jinsi wajumbe wa Kusadikika wanavyoweza kunasibishwa na wamisionari, wapelelezi au wafanyabiashara waliotumwa na mataifa ya Ulaya kwa maslahi ya mataifa hayo na jinsi walivyoweza kukumbana na masahibu mazito.

Kadhalika, kwa kupitia mjumbe wa Ardhi aliyejulikana kama Amini, bado tunaweza kushuhudia jinsi motifu ya safari inayofanywa na mhusika huyu inavyoweza kutumika kiistiara. Mwandishi anatufafanulia safari ya mjumbe huyu kama ifuatavyo:

> *Mjumbe aliyepatikana kwa safari hii, labda iliyo ya miujiza mikubwa sana kuliko zile zilizotangulia, alikuwa Amini. Amini alishuka katika Ardhi kwa msaada uliopatikana kwa hila kwa ndege Mangera, ndege wakubwa kabisa walishao katika Ardhi lakini walalao Kusadikika. Wakati wa kwenda chini Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la Mangera aliyekuwa amelala fofofo usiku. Kulipokucha ndege huyo aliruka mpaka chini. Alitua ziwani. Nusu ya mapaja yake ilikuwa majini. Kwa hivi Amini alijifungua, akaogelea bila kuonekana mpaka ufukoni. Ziwa hilo lilikuwa na maji baridi sana. Amini aliota jua mchana kutwa ili kuondoa mzizimo wa maji hayo. Hali yake ilipokuwa njema tena alizizuru pande zote za ardhi kama alivyotakiwa na kazi yake. Wakati wa kurudi Kusadikika mjumbe huyu alijifunga tena juu ya paja la Mangera aliyekuwa ameshughulika na kula*

> *karamu la mzoga wa ndovu bila ya kutazama huku wala huko. Safari hizi zilikuwa za ajabu na hatari kubwa kabisa. Amini hakutambua kama alichukuliwa na ndege mmoja au wawili katika safari hizi mbili* (kur.44-46).

Safari hii ya mjumbe wa Ardhi aliyejulikana kama Amini inatuhitimishia jinsi wajumbe walivyojitolea kwenda sehemu mbalimbali kwa hiari yao kujifunza maendeleo ili kuistawisha nchi yao. Kimsingi, safari hizi za wajumbe zimetumika kiistiara, safari ambazo zinaweza kunasibishwa na safari halisi zilizofanywa na wamisionari, wapelelezi na wafanyabiashara waliotumwa na mataifa ya Ulaya kuzizuru nchi mbalimbali ambazo baadaye yalikuja kuzitawala. Masahibu wanayokumbana nayo wajumbe wa Kusadikika yananasibishwa na masahibu yaliyowakumba wazungu hao wa mwanzo.

Katika kumalizia, tunaona jinsi istiara ilivyotumika katika kuusawiri ukoloni na jinsi wakoloni walivyokuwa walafi kiasi hata cha kujisababishia maangamizi kati yao. Maangamizi haya yanatokana na hali ya ubinafsi ambapo kila taifa lilitaka kujilimbikizia rasilimali zote zilizopatikana katika makoloni na hali hii inasemekana ni miongoni mwa sababu zilizosababisha hata kutokea Vita vya Kwanza vya Dunia na hata Vita vya Pili vya Dunia, vita ambavyo kwa namna moja au nyingine vilitikisa pande zote nne za dunia. Katika kulisawiri suala hili, mwandishi anatuambia:

> *Majuju ni taifa lafi na litishalo kabisa. Kila kitu kigumu kijulikanacho duniani kilikuwa ni laini kama mkate kati ya meno ya Majuju; na kilicho kichungu kilikuwa kitamu kama asali katika maonjo yao. Kwa ulafi uliokithiri viumbe hawa, walikuwa hawajui halali wala haramu. Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amekaa kitako mdomo wazi. Mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana. Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepa kinywa hicho. Tani milioni moja za mwamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo, na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani pia kila dakika tano. Lakini kila dakika moja Jeta alilia:'Kiu, njaa, kiu, njaa! Mfalme alitaka kumla Kabuli bila ya kugawana na wawinda waliomkamata. Choyo chake kikubwa kiliwaudhi wawinda, pakatokea vita baina ya majeshi ya mfalme na raia. Kwa vita hivyo kila kitu kilichokuwa na uhai kiliangamizwa, akabakia Kabuli peke yake.*
>
> *... Kabuli alipokuwa akilichimba kaburi lake kwa kisigirima, jembe lililochakaa, ilichimbuka johari kubwa na nzuri sana. ... Adhabu yake ya kwanza ilipokwisha, alitoka nje akawaonyesha askari waliokuwa wakimlinda johari aliyoigundua. Kwa kuona hivi, kila askari aliidai kuwa johari ile ilikuwa yake. Pale pale palitokea pigano kati yao lililowasukuma wote wawili katika kaburi lililokuwa wazi, wakatumbukia ndani yake kwa mshindo mkubwa sana. Mshindo huu uliufanya mchanga wa pande zote nne*

*juu ya kaburi kubomoka na kuwaelemea juu yao. Walikufa wakati ule ule* (kur. 25-27)

Tunaporejelea mandondoo hayo hapo juu kwa mfano, tunaona jinsi wakoloni walivyobeba maelfu ya tani za rasilimali mbalimbali yakiwemo madini mbalimbali kama vile dhahabu, almasi na shaba na hata mchanga wa migodini na kuupeleka kwao. Pia, walichukua rasilimali nyingine kama wanyama, ndege na vitu vingine. Kwa jumla, tamaa ya kujilimbikizia rasilimali hizi zilizokuwa zikipatikana Afrika zilisababisha migongano mikubwa sana miongoni mwa mataifa ya Ulaya hususani baada ya mapinduzi ya viwanda. Hebu angalia kwa mfano, Kabuli alikuwa akilindwa na askari wawili. Askari hawa wawili wanawakilisha mataifa mawili makubwa yaani Uingereza na Ujerumani. Chanzo cha kutokea kwa Vita vya Kwanza na vya Pili vya Dunia kulitokana na mataifa haya mawili yaliyokuwa na nguvu kwa wakati huo kutaka kutawala makoloni na kumiliki rasilimali zilizokuwa katika makoloni hayo. Johari iliyogunduliwa na Kabuli mle kaburini inawakilisha madini yaliyogunduliwa katika nchi za Kiafrika ambayo yalichochea kutokea kwa vita hivyo vikuu. Pigano kuu linalozungumziwa hapa lilikuwa ni vita vya dunia ambapo mshindo au athari za pigano/mapigano zilifanya mchanga wa pande zote nne juu ya kaburi kubomoka, yaani athari za vita vikuu vya dunia zilijitokeza katika pande zote nne za dunia; Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi.

**Hitimisho**

Shaaban Robert ni mwandishi nguli kabisa, ni mwandishi ambaye katika utunzi wa riwaya hii ya *Kusadikika* alitumia mbinu ya uhalisiamazingaombwe kwa lengo la kukwepa kile alichokuwa akikizungumzia kisiweze kubainika. Inawezekana kwamba, matumizi ya mbinu hii hayakutokea kwa bahati mbaya bali alikusudia kabisa kutumia mbinu hii ili kufikisha ujumbe. Matumizi ya mbinu hii yalikuwa na lengo la kumwepusha na suala zima la udhibiti wa kazi yake na pia kujiepusha na mkono wa dola kwa kipindi hicho cha ukoloni hasa tukikumbuka kwamba riwaya hiyo iliandikwa mwaka 1951; bado ikiwa ni kipindi ambacho nchi za Kiafrika zilikuwa chini ya ukoloni. Kwa kuchambua istiara zilizotumika katika riwaya hii na huku tukiongozwa na nadharia ya udenguzi iliyoasisiwa na Derrida (1967) ni dhahiri kwamba mambo yaliyoelezwa katika makala haya ni mambo yaliyojitokeza katika kipindi cha ukoloni na pia bado yanaendelea kujitokeza katika dunia ya leo.

Aidha, maelezo yote kuhusiana na historia ya Shaaban Robert tumeyachukua kutoka katika kitabu cha *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert* kilichoandikwa na Chuachua (2011). Kitabu hiki ni matokeo ya utafiti alioufanya ikiwa ni sehemu ya kukamilisha mahitaji ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma (2010). Tumeshawishika kutumia kazi hii kwa kuwa inahusisha utafiti halisi uliofanywa na mwandishi huyu na kwa hivyo ni imani yetu kuwa taarifa alizozitoa zina asilimia kubwa ya kuaminika.

Kwa upande wa istiara, tumejaribu kukiangazia kipengele cha istiara kama kilivyotumiwa na Diegner (2002) alipokuwa akitazama istiara katika riwaya za

awali za Euphrase Kezilahabi, makala yanayopatikana katika *Swahili Forum*, *AAP 72*. Kimsingi, kwa kupitia makala ya Diegner, nilishawishika sana kuchunguza namna waandishi wa mwanzo wa kazi za fasihi walivyoandika kazi zao kiistiara. Niliamini kuwa kwa kuwa Shaaban Robert ni kati ya watunzi wakongwe walioanza kuandika kazi zao kipindi cha ukoloni, basi ni dhahiri kabisa kazi zake za mwanzo ikiwemo hii ya *Kusadikika* haikuwa na budi kuandikwa kiistiara ili kujiepusha na mkono wa dola kwa kipindi hicho.

**Marejeleo**


Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Diegner, L. (2002). "Allegories in Euphrase Kezilahabi's Early Novels". AAP 72: *Swahili Forum* IX. pp 43-74.

Herman, L. (2012). "Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto," katika *Kioo cha Lugha*. *Juz. 10*. 122-123. Dar es Salaam: TATAKI.

Mlaga, W. (2013). "Riwaya ya Kiswahili katika Ufundishaji wa Historia," katika *Kiswahili*. *Juz. 76*. 38. Dar es Salaam: TATAKI.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*; *Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*, Dar es Salaam: KAUTTU.

Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth Literary Theory*. Kampala: Mukono Bookshop Printing and Publishing Company Ltd.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Robert, S. (1951). *Kusadikika*, Nairobi: Nelson.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*, Dar es Salaam: KAUTTU.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.